



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Simu. Na. 220 2325/2261  
Na. 220 2472  
E-mail: [ded@lindidc.go.tz](mailto:ded@lindidc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,  
306 Barabara ya Masasi,  
S. L. P. 328,  
**65183 MTAMA-LINDI.**

Kumb. Na.MDC/M.13.87/5

04/04/2025


Mkurugenzi Mtendaji,  
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC),  
SLP 938,  
**DAR ES SALAAM**

**YAH: UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS LIMITED  
(VCSL)**

Rejea somo tajwa hapo juu.

1. Naitambulisha kwako Kampuni tajwa hapo juu, ambayo ina malengo ya kuwezesha Vijiji mbalimbali hapa Tanzania katika kutekeleza Biashara ya Kaboni kupitia Mfumo unaojulikana kama “Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na Ukataji Miti hovyoy na uharibifu wa Misitu” (MKUHUMI).
2. Mpango huu unasaidia utunzaji wa Misitu ya Asili inayomilikiwa na Vijiji, kwa Mujibu wa Vifungu namba 4 (c) (i), 32 (1) (a) na (b) na 35 (6) (b) vya Sheria ya Misitu sura ya 323 ya Sheria za Tanzania.
3. VCSL inashirikiana na Vijiji na Halmashauri ya Mtama kutekeleza MKUHUMI, kwa lengo la kuzalisha na kuuza krediti za Kaboni, ambapo vijiji vitapata Fedha zitakazosaidia Maendeleo ya jamii hususani kuboresha Kilimo, Elimu ya Sekondari na Ufundi, Afya, Maji na upatikanaji wa Hati miliki za Ardhi.
4. Mradi wa VCSL inajulikana kama *Village Climate Solutions Project (VCSP)* na umesajiliwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais na Mfumo wa Kimataifa wa Viwango vya Kaboni (*Verified Carbon Standards - VCS*) na Viwango vya Ubora (*Climate, Community and Biodiversity – CCB standards*) kupitia akaunti namba 1325.

5. Katika Wilaya yetu, Mradi huu unatekelezwa katika Vijiji vifuatavyo (Ramani imeambatishwa)
  - i) Chiwerere
  - ii) Liganga
  - iii) Mihima
  - iv) Muungano
  - v) Nndawa
  - vi) Ntene
6. Tunawaomba Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kushirikiana na kampuni hii katika masuala yote yanayohusiana na uwekezaji na utekelezaji wa Mradi huu ili kuhakikisha mafanikio yake na manufaa kwa jamii.
7. Natanguliza Shukrani za dhati.
8. Wako katika utumishi,

  
Anderson D. Msumba,  
Mkurugenzi Mtendaji,  
**Halmashauri ya Wilaya ya Mtama.**

**Nakala:**

Katibu Tawala Mkoa,  
9 Barabara ya Mtuleni,  
S.L.P 1054,  
**65180 CBD LINDI.**

MKURUGENZI MTEENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
MTAMA

Katibu Tawala Wilaya,  
1 Barabara ya Majani Mapana,  
S.L.P 1020,  
**LINDI.**